## Abstract:

Utafiti huu ni jaribio la kuchanganua kishazi nornmo cha Kiswahili Sanitu. Kishanzi ni kishazi tegemezi ambacho huelekea kuchukua majukumu ya kirai nommo katika sentensi. Kazi hii imegawika katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa kazi yenyewe. Katika utangulizi huu tumeelezea sababu zetu za kuchagua mada na kuorodhesha madhumuni ya utafiti huu. Isitoshe. tumeufafanua msingi wa nadharia tuliyotumia na kupitia yaliyoandikiwa kuhusu mada tunayoishughulikia. Katika sura ya pili, tumetoa muhtasari wa maelezo ya dhana za kisarufi tunazoshughulikia kwa njia moja au nyingine. Katika sura ya tatu, tumeainisha kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu katika kategoria tatu na tukatoa ufafanuzi wake. Pia tumezitathmini nafasi za kisarufi zinazochukuliwa na kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu. Sura ya nne imeshughulikia upatanisho wa kisarufi t wa kishazi nomino cha Kiswahili Sanitu na kishazi kikuu na sura ya tano ni hitimisho ambapo tumeelezea tuliyoyatambua na kutoa mapendekezo.